JINA…………………………………….NAMBARI ………………DARASA…………..

**<u>102</u>**

# <u>KISWAHILI</u>

**NOVEMBER 2021**

**MUDA : SAA 2**

# <u>KIDATO CHA KWANZA</u>

**<u>MAAGIZO: Jibu maswali yote</u>**

**SEHEMU YA A: INSHA . (ALAMA 20)**

Fafanua namna ajali za barabarani zinaweza kuzuiwa nchini Kenya.

**SEHEMU B: SHAIRI (ALAMA 15)**

***Soma ushairi ufuatao kisha ujibu maswali.***

## Kila mdharau chake

Kuzimu wenda kuona, kila mdharau chake
Cha kwake akikana, kutumai cha mwenzake
Fahamu anayo laana, mpiga chake mateke
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona

Siringe na kujivuna, chako ukakipa teke
Unavunja lako jina, ili watu wakucheke
ana laana kwa Rabana, kila mdharau chake
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona

Awe Fatu na Amina, au Asha ndugu yake
Katu hawatafanana, kila mtu hadi yake,
Kila mjuzi wa mana, huwa hadharau chake
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona

Tama naomba amina, kilicho chetu tushike
Kidumu na kulingana, na tukipe hadhi yake
Ana laana kwa Rabana, kila mdharau chake
Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona

(*Diwani ya Akilimali na Akilimali Snow-White, K.L.B*)

**Maswali:**

1. Elezea ujumbe unaojitokeza katika ushairi huu. (al 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

2. Nakili kibwagizo cha ushairi huu. (al 1)

……………………………………………………………………………………………………………

3. Elezea aina za ushairi huu kwa kuzingatia: (al 6)

i. mishororo

………………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

ii. vina

……………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

iii. vipande

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

4. Elezea mambo matatu ambayo mshairi anatuonya dhidi yake. (al 3)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

5. Elezea maana ya maneno haya: (al 3)
   a. siringe

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

   b. katu

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

   c. hadhi

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**SEHEMU YA C: MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a. Elezea tofauti kati ya sauti /d / na / z/ (al 2)

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………

b. Onyesha silabi inayowekwa shadda katika maneneo haya. (al 3)
   i. umio

   ii. kinywa

   iii. mmomonyoko

c. Tunga sentensi moja ukitumia nomino ya kitenzi jina. (al 2)

…………………………………………………………………………………………………………

d. Andika sentensi ifuatayo kwa wastani. (al 2)

Magoma hayo yatachezwa mawanjani.

…………………………………………………………………………………………………………

e. Tambua viambishi awali na tamati katika neno: (al 3)

Achezaye

…………………………………………………………………………………………………………

f. Taja vipashio vya lugha kisha utolee mfano kwa kila kipashio:

(al 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

g. Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari. (al 2)

<u>Naam</u>, amekula <u>kichache</u>

……………………………………………………………………………………………………..

h. Jaza pengo kwa kutumia kinyume sahihi cha kitenzi kilichopigiwa mstari. (al 2)

i. Mimi nilim----------------- kunguru aliyokuwa <u>amenaswa</u>.

ii. <u>Alivaa</u> sare asubuhi kisha ------------------ jioni

i. Tunga sentensi moja kubainisha maana mbili za neno: chuo (al 2)

…………………………………………………………………………………………………………

j. Onyesha KN na KT katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Mpishi yule hodari atatuzwa vizuri sana.

k. Tunga sentensi **tatu** kudhihirisha matumizi mawili tofauti ya kibainishi. (al 3)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………..

l. Elezea maana ya kiimbo (al 2)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

m. Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (al 2)

Hao wenyewe hawakusomea mafunzo ya ukulima bora.

………………………………………………………………………………………………………….

n. Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya kielezi . (al 2)

…………………………………………………………………………………………………………

o. Bainisha ngeli za majina haya. (al 3)

i. zeruzeru

ii. ugwe

iii. saa

p. Yakinisha: Hukuja kunitembelea kazini. (al 2)

………………………………………………………………………………………………………..

q. Kamilisha methali: (al 2)

Maiti haulizwi ---------------------

**SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI (ALAMA 15)**

i. Taja vipera vine vya semi. (al 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………..

ii. Eleze:

A .Sifa za semi (al 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

B.Umuhimu wa semi (ala4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

iii. Elezea maana ya nahau hizi. (al 2)

a. kukunja jamvi ------------------------------------------------------------------

b. kupata jiko ------------------------------------------------------------------

iv. Fanani ni nani katika fasihi simulizi? (al 1)

…………………………………………………………………………………………………………………

**SEHEMU E: ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

Elezea sifa **<u>tano</u>** za sajili ya hospitalini.

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………